Set Light Exams School Based

# KISWAHILI LUGHA

CODE:20230304

CBC

JARIBIO LA MTIHANI **MWAKA 2023: GREDI 3**

## *Nakala ya Mwanafunzi*

**Jina la Mwanafunzi** ______________________

**Nambari ya mwanafunzi** [ ][ ][ ][ ][ ] **Tarehe**____________

**Jinsia:** ✓ **Mvulana** [ ] **Nambari ya Kaunti** [ ]

**Jina la shule:**______________ **Nambari ya shule** [ ][ ][ ][ ]

## Viwango Vya Kutathmini

| | Kuzidisha matarajio | Kufikia matarajio | Kukaribia matarajio | Mbali na matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kusoma kwa sauti | Anauwezo wa kusoma kwa kasi bila kusita. Anazingatia alama zote za uakifisho. | Ana uwezo wa kusoma bila kusita. Anazignatia baadhi ya alama za uakifisho. | Ana uwezo wa kusoma bila kusita. Hazingatii alama za uakifisho. | Hana uwezo wa kusoma maneno mengi. Hazingatii alama za uakifisho. |
| Kusikiliza na kuzungumza | | | | |
| Ufahamu | | | | |
| Sarufi | | | | |
| Kusoma kwa Sauti | | | | |

GREDI YA 3 / SHUGHULI ZA KISWAHILI

**ZOEZI 1.**

**KUSIKILIZA NA KUONGEA** **(alama 5)**

Mimi ninapenda runinga kwa sababu huniburudisha, hunichangamsha na kunielimisha. Sisi tunazo runinga mbili. Televisheni hizi mbili huwa sebuleni.

Kipindi nikipendacho ni kile cha Tugutuke ambacho hupeperushwa hewani kila Jumatano. Nahodha ama mtangazaji katika kipindi hicho huwa bwana Mumba mwenyewe. Kipindi cha Tugutuke huwa hewani kuanza saa mbili hadi saa mbili na nusu usiku. Je wewe wakipenda kipindi kipi?

**Maswali**

a). Kwa kina mwandishi kuna televisheni ngapi? ____________

b). Mwandishi hupenda kipindi kiitwacho? ____________

c). Kipindi akipendacho mwandishi huwa hewani kila siku ya ________

d). Mtangazaji katika kipindi kilichotajwa ni ____________

e). Jina lingine la mtangazaji ni ____________

**ZOEZI 2.**

**KUSOMA KWA SAUTI** **(alama 5)**

Bwana Kisere hufanya biashara kadhaa. Katika soko ya Makasa. Yeye hununua nyama katika kichinjio. Akiziuza nyama yeye hupata faida kubwa kwani anawateja wengi.

**ZOEZI 3: SARUFI** **(alama 20)**

**Andika majina ya picha hizi** **(ala 4)**

a)



____________

b)



____________

c)



_______________

d)



_______________

(Bakuli, baiskeli, shoka, kuku)

**2. Unda maneno ukitumia sauti hizi (ala 3)**

(a) ng ____________________

(b) sh ____________________

(c) ch ____________________

**3. Kanusha**

a) Mgeni alikuja ____________________

b) Mtoto analia ____________________

**4. Kamilisha sentensi kwa kutumia**

| **"huyo" ama "hao"** |
|---|

(a) Kuku ______ ndiye wa kaka

(b) ______ ndio wageni tuliowangoja

**5. Kamilisha sentensi kwa kutumia**

| **"-angu" ama "-etu"** |
|---|

(a) Mikoba hii siyo ________
**(zetu, yetu, wangu)**

(b) Kamba ya babu _______ imepotea
**(wangu, wetu, yetu)**

(c) Visima vile pale ni __________
**(changu, vyangu, chetu)**

(e) Nguo ________ imeshonwa vibaya
**(langu, zetu, yangu)**

**6. <u>Andika kwa maneno</u> <u>(ala2)</u>**

(a) 69 ____________________

(b) 38 ____________________

7. **Andika wingi** (ala 3)

(a) Karatasi ______________________

(b) Rubani ______________________

**ZOEZI 4.**

**UFAHAMU** (ala 5)




Katika kijiji kimoja cha Kalu paliishi mzee mmoja na familia yake. Mzee huyo alijulikana kama Bidii kwani alikuwa akijikaza kazini mwake. Hata hivyo wanawe wawili walikua wazembe kupindukia. Kataa na Zembe waliuendeleza uzembe wao hadi shuleni. Hawakuielewa methali, 'Mtaka cha mvunguni sharti ainame". Mama yao Bi. Maria alijaribu kuwarekebisha lakini hakufaulu.

Mwishowe wanawe walipata matokeo duni katika mtihani wa kitaifa.

**Maswali**

1. Mzee Bidii alikuwa na watoto wangapi? ______________________

2. Wanawe Mzee Bidii waliitwa

   ______________ na ______________

3. Mkewe Mzee Bidii alijulikana kama?

   ______________________________

4. Mzee Bidii na familia yake waliishi katika kijiji cha ______________________

**ZOEZI 5.**

**KUANDIKA** (ala 5)

**Ziandike sentensi tano utakazo somewa na mwalimu wako**

(a) ______________________________

(b) ______________________________

(c) ______________________________

(d) ______________________________

(e) ______________________________